

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
BUNGE LA TANZANIA**

Simu: +255 026 23222761-5
Fax No. +255 026 2322624
E-mail: cna@bunge.go.tz



Ofisi ya Bunge,
S.L.P. 941,
DODOMA.

TAARIFA KWA UMMA

Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria imepanga kupokea maoni ya wadau kuhusu **Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na.3 wa Mwaka 2020 (The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No.3) Act, 2020** kwa mujibu wa Kanuni ya 84(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016. Muswada huo umesomwa kwa mara ya Kwanza Bungeni tarehe 05 Juni, 2020.

Kamati imepanga kupokea maoni ya wadau kuhusu Muswada huo kuanzia siku ya leo **Ijumaa tarehe 5** hadi **Jumapili tarehe 7 Juni, 2020.**

Kwa kuzingatia umuhimu wa Muswada huo, Kamati inawaalika wadau wote kuwasilisha maoni yao kabla haujapelekwa katika hatua nyingine. Maoni ya wadau yanaweza kuwasilishwa kwa njia ya posta au Barua pepe kwa anuani ifuatayo:-

Katibu wa Bunge,
Ofisi ya Bunge,
S.L.P. 941,
DODOMA.

Barua pepe: cna@bunge.go.tz

Muswada huo pia unaweza kupakuliwa kupitia tovuti ya Bunge, www.bunge.go.tz

Imetolewa na: Kitengo cha Mawasiliano na Uhusiano wa Kimataifa,
Ofisi ya Bunge,
S.L.P 941,
DODOMA.

5 Juni, 2020.